

**AFRICA INLAND CHURCH (T)**  
**Taasisi ya Biblia na Utumishi**  
**Novemba 13-18, 2017**

**SOMO: THEOLOGIA YA KICHUNGAJI**

**MADA: KIONGOZI MWADILIFU. HITAJI KATIKA JAMII NA KANISA LA KRISTO,**

**UTANGULIZI:**

Familia inahitaji Kiongozi Kijiji vilevile kinahitaji Kiongozi, Kanisa hivyo hivyo linahitaji Kiongozi.

Lakini ni Kiongozi wa aina gani anayehitajika? Kiongozi **mwadilifu!**

Katika somo letu hili la Theologia ya Kichungaji tutaipitia Mada hii Kiongozi Mwadilifu kwa kuona Neno la Mungu linasema nini juu ya uadilifu na Kiongozi mwadilifu. Neno la Mungu litakuwa msingi wetu juu ya mada hii.

**Pengo la kutokuwa na Kiongozi**

- ✓ Waamuzi 21:25- hapakuwa na mfalme katika Israeli na kila mtu alifanya yaliyokuwa ni mema machoni pake mwenyewe.
- ✓ Waamuzi 18:1- Siku hizo hapakuwa na mfalme katika Israel – kabila la wadani walijitafutia urithi wao wenyewe kwa utaratibu wao wenyewe
- ✓ Kitabu hicho hicho cha Waamuzi , kinataja juu ya kuinuka kizazi kisichomjua Mungu. Waamuzi 2:10
- ✓ Nabii Amosi kwa upande wake anazungumza juu ya njaa ya kulikosa Neno la Mungu katika taifa la Israeli Amosi 8:11-12  
Hali hii iliashiria kukosekana kwa viongozi waadilifu.
- ✓ Mfalme Sauli katika kipindi chake alitafuta neno toka kwa Bwana, lakini hakulipata. Isam 28:5-6
- ✓ Tendo la kutokupa neno toka kwa Bwana, lilimfanya Sauli atafute njia nyingine, nje ya mpango wa Mungu. Isam 28:7-17

**Mungu ni Chimbuko la Uadilifu**

“Yeye Mwamba, kazi yake ni kamilifu; maana njia zake zote ni haki. Mungu wa uaminifu asiye na uovu, Yeye ndiye mwenye haki na adili. Kumb 32:4.

Wito wa Mungu kwa watu wake ni Mika 6: 8, Zab 89: 14, Zab 85:10, Zab 9:7f, 96:10-13 angalia pia Mithali 14:31,17:5.

**Mungu aliye Chimbuko la Uadilifu anatutaka tufanye nini kama watoto wake**

**(Mjadala katika vikundi)**

---

---

---

---

---

---

---

---

**Uadilifu ni jambo linaloweza kukupapaswa katika jamii.**

Fafanua mjadala katika vikundi

---

---

---

---

---

Kiongozi anatazamiwa kuwa na uwezo wa kushawishi watu ili wamfuate. Njia ipi iliyo na ushawishi zaidi katika hizi mbili:

- 1) Maneno yenye ushawishi
- 2) Maisha ya Uadilifu ya Kiongozi. Eleza

---

---

---

---

---

---

---

---